TANGAZO LA SERIKALI NA. 458 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA UHIFADHI WA MISITU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Uhifadhi wa Misitu ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni maana yake ni Afisa Maliasili, Afisa Misitu, Afisa Wanyamapori, Afisa nyuki, wasaidizi misitu pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Eneo la Hifadhi" ni maeneo ya Milima, Mbuga za Wanyama, Maeneo ya vyanzo vya Maji, Hifadhi ya Misitu, Miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilaya ya Hai;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"Kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa au kuongezewa thamani;

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au

kung'oa miti,visiki;

Sura ya 191 "maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira ;

Sura ya 191 "maji taka" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 323 "mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya misitu;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anaejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai;

Sura ya 191 "mazingira" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 323 "Misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Misitu;

"taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "taka za viwandani" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "uchafu Hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "uchafuzi wa mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "udongo" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "vitu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"Miti iliyohifadhiwa" ni pamoja na Mvule, Mkufi, Mninga, camphor (Kafuri), ikiwa ni miti yote iliyotangazwa au itakayotangazwa katika gazeti la Serikali;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Kuchoma au kusababisha moto

4.-(1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchoma au kusababisha moto katika eneo la Misitu ndani ya Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, Kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha,

mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

5.-(1) Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma moto siku saba kabla ya kuchoma, na atatakiwa kuweka njia za kuzuia moto.

Ukataji miti

6.-(1) Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa au maeneo binafsi kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka kwa Afisa Misitu.

(2) Wataalamu wa Misitu watatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

(5) Mtu yeyote atakayevuna miti ya asili na au iliyohifadhiwa kisheria atatakiwa kulipia ushuru wa asilimia 5 kulingana na miongozo iliyopo baada ya vipimo vya ujazo wa mti kuchukuliwa na wataalamu.

Wajibu wa kupanda miti

7. Kila Mkazi wa Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri na kushiriki katika kampeni za upandaji wa miti katika Wilaya, Kata au kijiji chake anakoishi.

Utaratibu wa kupata kibali cha kukata mti

8.-(1) Mtu yeyote anayetaka kukata mti au miti:,

(a) atatakiwa kuandika barua kwenda kwa Mtendaji wa Kijiji ikionyesha nia ya kukata mti au miti;

(b) maombi hayo yatajadiliwa na Kamati ya Mazingira ya Kijiji husika, na yakikubaliwa yatapelekwa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kwa ajili ya kuidhinisha kibali cha kukata miti.

(c) kama maombi yake yatakataliwa atajulishwa kwa

maandishi sababu za kukataliwa.

(2) Kibali kitakachotolewa kwa ajili ya kukata mti au miti kitadumu kwa siku saba.

Udanganyifu

9.-(1) Mtu yeyote ambaye atadanganya kuwa ana kibali cha kukata miti wakati hana kibali hicho ikithibitika atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo

(2) Afisa ambaye atashindwa kusimamia vibali vya ukataji miti au atatumia vibali ambavyo havijafuata taratibu ikithibitika Afisa huyo atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Eneo la hifadhi ya misitu

10.-(1) Kila kijiji kitatenga eneo la hifadhi ya Msitu kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

(2) Kila kijiji kitatunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji.

(3) Kila Kijiji kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake kutokana na ushauri wa wataalam.

(4) Mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumzi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughulli nyinginezo, atatakiwa kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Afisa Maliasili au Misitu wa Wilaya baada ya kuwasilisha maombi kupitia kwa Mtendaji wa kijiji husika kwa maandishi na kukaguliwa kama yamekidhi vigezo.

(5) Ni marufuku kutumia msumeno wa moto (Chain saw) usiokuwa na usajili kwa kuchana mbao katika maeneo yote ya Halmashauri.

(6) Kila Kijiji kinatakiwa kupanda miti isiyopungua 15,000 na kuitunza.

(7) Kila Shule au Taasisi yoyote katika Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti 1000 kwa matumizi ya Shule au Taasisi husika.

(8) Kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.

(9) Kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo.

(10) Kila Mwenye Nyumba atawajibika kupanda miti kwenye eneo lake na kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza.

Hifadhi ya vyanzo vya maji

11.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila Halmashauri kupanda miti iliyo rafiki na Mazingira katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu na Afisa Mazingira.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri husika pekee.

(4) Ni marufuku mtu yeyote kuchimba mchanga au kuondoa mawe eneo lolote la mto, chanzo cha maji au eneo lolote la hifadhi bila kuwa na kibali kutoka mamlaka zinazotambuliwa na Serikali.

Taratibu za kilimo

Sura ya 113
Sura ya 114

12.-(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa Mwidhiniwa kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Masharti kwa Mkulima

13.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, bwawa na ziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya Misitu au Mazaingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa wa Kilimo na wa wataalam wengine wa Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba lililo karibu na misitu au hifadhi ya mazingira kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka Halmashauri.

(3) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(4) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia saa 12:00 Asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi.

(5) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za

Kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia Kilimo cha kuhamahama na kuhimiza Kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Uhifadhi wa uoto wa asili

14. Kila mkazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika umeharibiwa, ana wajibu wa kuhakikisha kuwa analirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji wa mchanga na kokoto

15.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga au kuondoa mawe katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa, kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

Makosa na adhabu

16. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;-

(a) atavuna au atauza mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hii;
(b) atanunua mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hii;
(c) atasafirisha mazao ya misitu bila ya kuwa na nyaraka;
(d) atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hii;
(e) atakataa au kushindwa kutii maagizo ya Afisa Mwidhiniwa;
(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Mtumishi yeyote wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii;
(g) atatishia uhai wa Mtumishi wa Halmashauri au Afisa Mwidhiniwa wakati akitekeleza majukumu yake;
(h) atalazimisha kupita katikaa vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu kwa nguvu bila kukaguliwa;
(i) atatumia msumeno wa moto usiokuwa na usajili katika shughuli zote za uvunaji wa miti;
(j) ataendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya biashara kutoka Halmashauri;
(k) atanunua mazao ya misitu bila kulipa ushuru wa mazao ya misitu wa asilimia 5 kwa Halmashauri;
(l) atanunua, kuuza au kutorosha mazao ya misitu kwa

madhumuni ya kukwepa masharti ya Sheria Ndogo hii;

(m)atasafirisha mazao ya misitu bila kulipa ushuru.

17. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua elfu hamsini kwa kila kosa na isiyozidi Milioni moja kwa kila kosa au kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili au adhabu zote kwa pamoja, yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 12 mwezi Mei, mwaka .

DIONIS M. MYINGA
*Mkugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Hai*

EDMUND RUTARAKA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Hai*

NAKUBALI,

**L.S**

Dodoma,
5 Disemba, 20243

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*